**BARUA YA WAZI YA UMOJA WA WAFANYABIASHARA NDOGO NA ZA KATI TANZANIA KWENDA KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DK. SAMIA SULUHU HASSAN**

**Anuani ya Posta: 15788, Dar es Salaam**
**Simu: +255 22 2180668**

**Tarehe 13 Novemba 2025**

**Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan,**
**Amiri Jeshi Mkuu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,**
**Ikulu, 1 Barabara ya Julius Nyerere, Chamwino, Dodoma, Tanzania.**

**YAH: MATUKIO YA OKTOBA 29 NA OKTOBA 30, 2025 KATIKA BAADHI YA MAENEO MBALIMBALI NCHINI**

**Mhe. Rais,** Kwa unyenyekevu mkubwa, sisi wamiliki wa biashara za kati na ndogo nchini tumechukua uamuzi wa kukuandikia barua kutokana na matukio yaliyoambatana na vurugu na uharibifu yaliyotokea katika maeneo kadhaa hasa ya mijini kwenye mikoa mbalimbali nchini kati ya alasiri Oktoba 29 hadi jioni Oktoba 30, 2025.

**Mhe. Rais,** katika matukio haya baadhi ya watu walipoteza maisha. Tunawapa pole wote waliopata misiba na roho za waliopoteza maisha zipumzike kwa amani.

**Mhe. Rais,** katika matukio yale sisi kwa umoja wetu tumepata changamoto kubwa sana kiuchumi ambayo imeathiri sio sisi peke yetu bali mamilioni ya wanaotutegemea kimaisha.

**Mhe. Rais,** wanasema anayeharibu sehemu unapopata riziki ni karibu sawa na anayechukua uhai wako. Baadhi yetu tumetumia sehemu kubwa ya maisha yetu na nguvu zetu kufika pale tulipokuwa kabla ya ghafla kupoteza karibu kila kitu kwenye vurugu zile. Wako baadhi yetu Mhe. Rais ambao hata wafanyakazi wao wa kike hasa kwenye kwenye maeneo ya burudani walikumbwa na matukio ya ubakaji. Imani yetu ni kuwa utapata taarifa zote hizi kupitia vyombo vyako rasmi vya kiusalama.

**Mhe. Rais,** wakati huu wengi wetu tuko kwenye msongo mkubwa sana wa mawazo, madeni na umaskini. Baadhi yetu ama wamelazwa hospitali kwa mshtuko au wanaugulia nyumbani lakini pia tume wanachama kadhaa waliopata umauti kwa mshtuko wa hasara za vurugu zile. Mhe. Rais, Sisi tuna maombi kadhaa kwako ambayo tunaamini wewe kama Amiri Jeshi Mkuu na Kiongozi Mkuu wa Nchi yetu pamoja na wasaidizi na washauri wako mtayachukua na kuyapa uzito;

**Moja,** Mhe. Rais tunaomba kwa hali yoyote na mbinu zote jambo hili la wizi na uharamia wa makundi katika miji na majiji lisijirudie tena ndani ya nchi yetu. Tunapoteza maisha, mali na kila aina ya hasara. Jambo hili limeturudisha nyuma na tunaomba ufanye kila lililo ndani ya uwezo wako kama Amiri Jeshi Mkuu nchi yetu iendelee kuwa salama. Sisi na wote wanaoutegemea tutakuunga mkono kwenye kila hatua ya kuhakikisha hili linafanikiwa.

**Mbili,** Mhe. Rais tunaomba kipaumbele katika kuyachukulia hatua za kisheria matukio ambayo wahusika wake wameonekana kwenye picha za kamera za ulinzi na klipu mbalimbali. Baadhi ya uharibifu uliofanyika umerekodiwa na wahusika wenyewe na sura zao ziko mitandaoni. Mhe. Rais tunaomba kuwe na kikosi kazi maalum kufuatilia watu hawa na kufikishwa mahakamani kwa kesi hizo ili walau tuweze kupata haki kwa kiasi fulani.

**Tatu,** Mhe. Rais tunakuomba wewe na Serikali yako kuona namna ya kutoa ombi maalum kwa mabenki, taasisi za mikopo na bima kutazama baadhi ya matukio haya kwa jicho la tatu na kuona namna inavyowezekana ama kupata baadhi ya fidia ama kuongezewa muda kwa wale wenye mikopo mbalimbali.

**Nne,** Mhe. Rais ziko biashara ambazo ni huduma za moja kwa moja na za msingi kwa jamii ambazo zimeharibiwa mfano zahanati, shule na hospitali. Tunatoa ushauri Mhe. Rais kwa biashara za aina hii kupewa fidia ya kimaafa si fedha bali ujenzi ili kuzirudisha kuleta huduma kwani waathirika wa kukosekana huduma kwa maeneo haya ni wengi.

**Tano,** Mhe. Rais ni kuhusu usafiri katika Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam ndilo kiungo muhimu cha uchumi wa nchi yetu na mzunguko wa fedha. Baada ya vurugu hizi usafiri mkubwa wa huduma ya mabasi yaendayo haraka imevurugika. Foleni zimekuwa kubwa katika barabara nyingi kwani usafiri wa mwendokasi haupo tena. Mhe. Rais tunaomba kama Kiongozi Mkuu wa Nchi yetu na Mama utazame namna ya haraka ya kurejesha usafiri huu. Kukosekana kwake kunaathiri sana maisha na biashara Dar es Salaam hasa kwa watu wa kipato cha kati na cha chini.

Mheshimiwa Rais, tunaomba kuhitimisha kwa sasa. Tuna imani kuwa utapokea maombi yetu kupitia barua hii na utaona yapi yanaweza kufanyika. Tunakuhakikishia ahadi yetu ya kuunga mkono kila hatua njema ambazo wewe, Serikali na vyombo vya ulinzi na usalama vya nchi yetu vitachukua kuhakikisha kuwa uharamia ule usio utamaduni wa Tanzania hautokea tena katika nchi yetu.

***Kwa heshima kubwa,***

***Sisi Wamiliki wa Biashara za Kati na Ndogo Tanzania.***

***Nakala:***

***Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania.***
***Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa.***
***Mkuu wa Jeshi la Polisi.***

***Katibu Mkuu***
***Wizara ya Biashara na Viwanda.***



*"Biashara ni huduma."*